# KWENYE MSALABA

Ijumaa Kuu

*Deogratius Rwechungura*
*St. Patrick - Vwawa Mbozi*




2. Kwenye Msalaba - atupa neema; Kwenye Msalaba - atuhurumia
   Laana ilotoka kwa Adamu ilifutwa kwa kifo chake Yesu Ee Msalaba .....
3. Kwenye Msalaba - atuosha dhambi; Kwenya Msalaba - atuacha huru
   Atulipia sote dhambi zetu kwa damu yake nyingi alomwaga Ee Msalaba ....
4. Kwenye Msalaba - katupa Mamaye; Kwenye Msalaba - katufanya ndugu
   Eva ndiye aliyeleta kifo uhai ukaletwa na Maria Ee Msalaba ....
5. Kwenye Msalaba - japo yu mkimya; Kwemye Msalaba - atupa fundisho
   Tukitaka kufika kwake Baba tuubebe na sisi Msalaba Ee Msalaba .....
6. Kwenye Msalaba - Yesu atuonya; Kwenye Msalaba anatuhimiza
   Wanangu tazameni pendo langu ni pendo la huruma kwenu ninyi Ee Msalaba....
7. Kwenye Msalaba - Mkombozi wetu; Kwenye Msalaba - atuita sote
   Njoni kwangu mfwate njia yangu katika raha pia shida zenu Ee Msalaba ....